# HOTUBA YA MHE PROF. MAKAME MBARAWA (MB), WAZIRI WA MAJI WAKATI WA UZINDUZI WA MRADI WA MAJI WA KIJIJI CHA SHILIMA, KATA YA KIKUBIJI, WILAYANI KWIMBA MKOANI MWANZA

TAREHE 14 SEPTEMBA, 2019

- Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mwanza.
- Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Kwimba.
- Waheshimiwa Viongozi wa CCM Mkoa wa Mwanza
- Waheshimiwa Viongozi wa CCM Wilaya ya Kwimba
- Mhe. Diwani wa Kata ya Kikubiji
- Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi ya MWAUWASA.
- Viongozi mbalimbali mliohudhuria hapa.
- Waandishi wa Habari.
- Ndugu wananchi mliojumuika hapa.
- Mabibi na Mabwana.

Ndugu Wananchi, Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema ambaye ametuwezesha kuifikia siku hii muhimu ya leo tukiwa na afya njema. Aidha nichukue nafasi hii kuwashukuru sana viongozi wote wa Chama na Serikali Mkoa wa Mwanza pamoja na Wilaya ya Kwimba kwa kunialika kuwa mgeni rasmi katika siku hii muhimu ya uzinduzi wa mradi wa maji katika kijiji hiki cha Shilima.

**Ndugu wananchi,** Ujenzi wa mradi wa maji katika Kijiji hiki cha Shilima ni utekelezaji wa Sera ya Maji pamoja na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) inayoelekeza kuwapatia huduma ya majisafi na salama kwa asilimia 85 wakazi wote waishio vijijini ifikapo mwaka 2020. Aidha mwaka 2015 wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli aliwaahidi Watanzania kuwa atafanya kila njia kuhakikisha kuwa tatizo la maji kwa wananchi wote linatatuliwa.

**Ndugu Wananchi,** Kijiji cha Shilima ni moja ya Vijiji 12 vilivyopo kwenye utekelezaji wa programu ya maji na usafi wa Mazingira Vijijini Wilayani Kwimba. Katika utekelezaji wa program hii, tayari vijiji vya **Ishingisha, Mwabilanda, Nyambiti, Milyungu, Nyanhinga, Hungumalwa, Igunghya na Igumangobo** vimeanza kutoa huduma ya maji na kusimamiwa na wananchi kupitia kamati zao za maji.

**Ndugu wananchi,** Nimetaarifiwa kuwa Kijiji cha Shilima kina wakazi wapatao 7,526. Mradi huu ambao tunauzindua leo umejenga magati 35 ambayo yana uwezo wa kuhudumia wakazi 8,750 ikiwa ni wastani wa watu 250 kwa gati moja. Kwa hiyo

mradi una uwezo wa huwahudumia wakazi wote wa kijiji hiki pamoja na Vijiji vya Jirani.

**Ndugu Wananchi**, Uzinduzi wa mradi wa Maji katika kijiji hiki cha Shilima ni awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi wa maji katika Vijiji vya **Shilimia, Mhande** na **Izizimba.** Nilipofika hapa tarehe 3 Julai, 2019 niliahidi kuwa tutahakikisha kuwa wananchi wa Kijiji cha Shilima mnapata maji katika kipindi cha miezi miwili (yaani hadi kufikia tarehe 3 Septemba, 2019). Ninafurahi kuona kuwa mlianza kupata maji tokea tarehe 25 Agosti ambapo ni kabla ya kipindi nilichoahidi. Ninachukua nafasi hii kuwapongeza sana viongozi wote hususani Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mkuu wa Wilaya, watendaji wa RUWASA, Viongozi wote wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuanzia ngazi ya Mkoa, Wilaya, Kata hadi Kijiji. Pia nawapongeza Bodi na Watendaji wa MWAUWASA kwa usimamizi mzuri wa kazi hii. Na mwisho niwapongeze sana wananchi wote kwa ushirikiano wenu katika utekelezaji wa mradi huu hususani wale waliofanya kazi za uchimbaji wa mitaro na ulazaji wa mabomba .

**Ndugu Wananchi,** Naomba niwaahidi tena kuwa kazi za ujenzi wa mradi katika vijiji vya **Mhande** pamoja na **Izizimba** zitaendelea kutekelezwa na kukamilika ndani ya kipindi cha miezi miwili

kutoka siku hii ya leo. Naomba sana tuendelee kushirikiana ili kazi hizo zikamilike kwa wakati tuliopanga ili kuhakikisha kuwa wananchi wote waishio vijijini wanapata maji kwa asilimia 85 ifikapo 2020.

**Ndugu wananchi,** Kama alivoeleza Meneja wa RUWASA Wilaya, mradi huu wa Shilima ulianza kutekelezwa mwaka 2013 na ulitakiwa kukamilika katika kipindi cha miezi sita. Lakini kutokana na udhaifu wa Mkandarasi pamoja na usimamizi mbaya, mradi huu haukuweza kukamilika kwa kipindi hicho na kusababisha wananchi kuendelea kuwa na shida kubwa ya upatikanaji wa maji. Baada ya kutambua hilo na kwa kushirikiana na Mhe. Mkuu wa Mkoa tuliamua kusitisha mkataba wa ujenzi na kumfukuza mkandarasi na tukaamua mradi ujengwe na wataalamu wetu wa ndani.

Aidha endapo kazi za umaliziaji wa ujenzi wa mradi huu zingefanywa na Mkandarasi, mradi ungegharimu takribani kiasi cha Tzs bilioni tatu. Lakini kwa kutumia wataalamu wetu wa ndani mradi huu utagharimu Tzs 2,008,755,000. Mpaka sasa kiasi cha TZS Milioni 564 zimeshatolewa na kiasi cha fedha kilichobaki kinatolewa mwezi huu. Fedha hizo zitatumika kukamilisha kazi katika Vijiji vya Mhande na Izizimba.

**Ndugu Wananchi,** pamoja na ujenzi wa mradi huu wa Shilima, Wizara pia inatekeleza Mpango wa Uboreshaji wa Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Ziwa Viktoria, yaani *Lake Victoria Water Supply and Sanitation Program* (LV WATSAN) ambao unatekelezwa katika miji sita ambayo ni Mwanza, Musoma, Bukoba, Magu, Misungwi na Lamadi kwa gharama ya Euro miioni 104.5 ambazo ni sawa na wastani wa TZS bilioni 276.

Katika fedha hizi, Shirika la Maendeleo la Ufaransa – French Development Agency (AFD) pamoja na Benki ya Uwekezaji ya Ulaya – European Investment Bank (EIB) zinachangia Euro milioni 90 sawa na TZS Bilion 238 ambazo ni mkopo wa masharti nafuu ambapo kila mmoja anachangia Euro million 45 sawa na TZS Bilioni 119 na Serikali inachangia Kiasi cha Euro milioni 14.5 sawa na TZS Bilioni 38.

Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi huu miradi yote katika miji ya Magu, Misungwi na Lamadi itaanza kutoa maji kwa wananchi.

**Ndugu Wananchi,** Naomba niwahakikishie Wakazi wa Mikoa yote inayozunguka Ziwa Victoria kuwa Wizara yangu imedhamiria kwa dhati kabisa kuhakikisha kuwa tatizo la maji katika ukanda huu wa ziwa Victoria na pande zote za nchi yetu linakwenda kuwa historia.

Baada ya kusema hayo nirudie tena kuwashukuru kwa dhati kabisa kwa ushirikiano wenu ASANTENI SANA.